# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZOYAKUJIUNGANAKIDATO CHATANOKATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAMISEMI**

**NambazaSimu………………**

**Mkuu wa Shule- 0655329798**

**Makamu Mkuu wa shule- 0657061332**

**Shule ya Sekondari BUNGU**

**S.L.P 514 KOROGWE-TANGA**

**Tarehe………………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………….**
**S.L.P……………………………………**

Yah:**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULEYA BUNGU SEKONDARI HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE MKOA WA TANGA MWAKA………………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwakujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………na atasoma tahasusi ya ……………

Shule ya Sekondari Bungu ipo umbali wa Kilometa 30 Kaskazini mashariki mwa Mji wa Korogwe Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Korogwe Nauli ni Shilingi 6,000/= kwa basi, kwa pikipiki Shilingi **15,000/=** na Tshs **30,000/=** kwa bajaji. Muhula wa Masomo unaanza tarehe 08/07/2025 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………………

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Sketi rangi ya orenji au karoti mbili mshono rinda box iwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu. Shona popote.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu au nusu kanzu kwa waislamu (watakaopenda kuvaa ) nunua popote.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) mbili nyeupe zifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. shona popote
iv. Track suti ya rangi ya kijivu yenye mistari mweupe yenye nembo kwa atakayehitaji inapatikana shuleni kwa gharama ya 23,000/=
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule
vii. Sweta rangi ya damu ya mzee nunua popote, ila unaweza kuipata shuleni kwa shilingi 12,000.00
viii. Nguo za kushindia (*shambadress*) rangi ya kaki mshono solo na kijuba cha kaki kwa waislamu (shona popote),
ix. Tai ndogo fupi rangi ya orange. nunua popote
x. Tisheti(T-shirt) rangi ya kijivu light, kwa atakayehitaji inapatikana shuleni kwa Tsh12,000)
xi. Jacket 1 jeusi
xii. Pull neck nyeupe 1
xiii. Pair moja ya kanga na taulo 1 la pink
xiv. Mashuka Jozi 3 (pinki 2 nyeupe 1*)*, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari(*counterbook quire3 kumi* );
ii. **Ream(A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vyama somo ya tahasusi husika(*orodhaitambatishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya kawaida yanayotumiwa na wanafunzi wa bweni.
vii. Mashuka Jozi 3 (pinki 2 nyeupe 1), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Nguo za michezo bukta na fulana ya taifa Stars black na raba nyeupe;
x. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe);

xi. Ndoo2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xii. Kwanja1 (HGK), jembe1(HGK, CBG), reki1 (CBG), rubber squeezer 1(CBG), na ufagio wa chelewa 1, (HGK), soft broom (HGK), brush rungu ya kusafishia chooni1(CBG),

xiii. Taa ya solar au kuchaji(kwa matumizi yake ya dharura)

**Vitabu vya kujisomea**

**HISTORY**

1History for secondary school form 5 and 6 by TIE

2. Essential history for secondary school paper 1 and 2 by Saleh Yasin

**GEOGRAPHY**

1. A Comprehesive approach to physical Geography by DT Msabila
2. Practical geography, map reading and photography advance level 5 and 6

**KISWAHILI**

1.Kiswahili –Lugha na Sarufi kidato cha 5 na sita by TIE

2.Kiswahili-Fasihi kidato cha 5 na sita by TIE.

**GENERAL STUDIES**

1. Historia ya Tanzania na Maadili

**CHEMISTRY**

1. Advanced physical chemistry 1 and 2(mzumbe book project)
2. Organic chemistry part A and B(mzumbe book project)

3.Inorganic chemistry 1and 2 (mzumbe book project

**BIOLOGY**

1 Advanced biological science.

2.Functional approach biology.

**ANGALIZO: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.**

**Michangombalimbali**

**a) ShulezaBweni**

| Na | AinayaMchango | Kiasi |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshajiwa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| Na | AinayaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**NB. Michango yote ya fedha iwekwe kwenye akaunti ya shule namba 41501100023 NMB BANK Jina la Akaunti ni Bungu Sec. Recurent Akaunt. Andika jina La mwanafunzi Katika Bank Pay Slip Upande wa mwekaji wa fedha. Mwanafunzi aje na Bank Pay Slip hiyo shuleni kuonyesha malipo aliyoyafanya**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu zaShule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwakikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
**xii.** Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele(**awe na nywele fupi)**

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya Mwana Funzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA;**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga na kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati,mahusiano ya jinsimoja,kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau BenderayaTaifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu

5. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

KARIBUSANAKATIKASHULE HII SainiyaMkuuwaShule.……………………………………… Jina la Mkuu wa Shule .……………………………………. MhuriwaMkuuwaShule ………………………………..

NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).
Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wamzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule -0655329798
- Makamu Mkuu wa shule- 0657061332

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE(V).

(B). REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

BUNGUSECONDARY SCHOOL, P.O.BOX 514, KOROGWE–TANGA. DATE…………………………………
Email: bunguhighschool2016@gmail.com

MEDICALOFFICER .......................................................................GOVERNMENT HOSPITAL.
NAME OF STUDENT………………………………..…………………………………………
Please examine the above-named student to ascertain his/her fitness for further studies.
……………………………………………………………………………………………………

HEAD O SCHOOL. MEDICAL CERTIFICATE:
[To be completed by the medical officer].
Ihave examined the above named students with regard to:
Skin……………………Eyes…………………Ear………………Chest…………..…Eyes…….………...
Spleen…………………..Abdomen……………………Urine……………………Stool………………….
Hemoglobin…………………Sickle cell……………………………others……………….………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

AndI considered.
He/She is good health,free from infection diseases,worms,bilharzias,and fit to go to school. He/She is now to return to school having treatment for
…………………………………………..….
Name& signature of medical officer
………………………………………………………………….. Date:…………………………

NB.JAZA FOMU HII NYUMBANI KABLA YA KUFIKA SHULENI AU SIKU YA KURIPOTI UNAPORIPOTI UWE NAYO.

**PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI AU NDUGU WATAKAO WASILIANA AU KUFIKA SHULENI KUMTEMBELEA MWANAFUNZI.**

| | |
|---|---|
| 1.PICHA | 2. PICHA |
| Majina matatu | Majina matuta |
| ………………………………. | …………………………….. |
| Uhusiano na mwanafunzi | Uhusiano na mwanafunzi |
| ………………………………. | ……………………………… |
| Simu…………………….. | Simu………………………… |
| 3.PICHA | 4.PICHA |
| Majina matatu | Majina matuta |
| ………………………………. | …………………………….. |
| Uhusiano na mwanafunzi | Uhusiano na mwanafunzi |
| ………………………………. | ……………………………… |
| Simu…………………….. | Simu………………………… |

**NB. HATUTARUHUSU MTU MWINGINE YEYOTE KUMTEMBELEA, KUFIKA SHULENI AU KUFANYA MAWASILIANO NA MWANAFUNZI**